Jina……. **Nambari yako……/……**

Shule…… **Sahihi yako……..……**

Tarehe ……..…

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(LUGHA)
JULY / AUGUST - 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MANGA - 2010

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(LUGHA)
JULAI / AGOST - 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1. Karatasi hili lina maswali manne. (Ufahamu, ufupisho, lugha na Isimujamii)
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

Karatasi hili lina kurasa 12 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.

UFAHAMU

1. **Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa ni kuitikia wito wa mataifa wa kupanua mawasiliano kati ya watu wa mataifa mbalimbali ili kuongeza uelewano kati ya jamii ya mwanadamu. Hadi hivi leo mawasiliano kati ya mataifa yamekuwa yakitawaliwa na lugha za magharibi kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani. Lugha nyingine kuu kama vile Kirusi, Kichina, Kiarabu na Kireno ama zimekuwa zikitoa huduma za mawasiliano katika mataifa yanayozaa lugha hizo au katika mataifa hayo pamoja na mataifa yenye aina fulani ya uhisiano huo. Lugha za aina ya kwanza zilitimiza mahitaji ya mawasiliano nyumbani halafu zikavuka mipaka ya mataifa yake na kutumiwa kama lugha za mataifa mengine.

Umataifa wa lugha hizi umekuwa wa kulazimisha: kwani kuingia kwa lugha hizi katika mataifa ya kigeni aghalabu kuliambatana na majilio ya ukoloni. Na katika laghba yao ya kueneza na kutukuza utamaduni wao, wakoloni wakaona lugha za kuzungumzia mambo nje ya mataifa yao hapana ila lugha za asili zao. Hivyo wachache wa wananchi watawaliwa walipoandaliwa kushiriki katika mifumo ya kikoloni waliandaliwa kwa lugha za wakoloni. Na hata baada ya kujitawala wananchi waliojaliwa kubabaisha elimu ya shuleni walijikuta hawana lugha nyingine ya kuwasiliana na mataifa ya kigeni ila lugha za wakoloni. Wakalazimika kuzitangaza lugha za wakoloni kuwa ni lugha rasmi za serikali zao na hata kuzipa hadhi ya lugha ya taifa pale ambapo ukoloni ulikolea sana.

Lugha za aina ya pili nazo kwa nguvu fulani fulani za utawala wake zililazimisha mataifa mengine yazitambue. Mathalani umuhimu wa mafuta ya petroli na mazao yake ulilazimisha mataifa yenye kutaka kunyonya utajiri wa mafuta hayo yajue wayasemayo Waarabu. Hivyo Waarabu wakapatiwa uhuru wa kutumia Kiarabu katika vikao na kumbi za kimataifa. Warusi nao, kwa kutetea imani ya kijamaa na kutekeleza kwa matendo baadhi ya imani hizo, wakawa tishio kubwa kwa mataifa ya kibepari. Hivyo kila kilichosemwa kwa Kirusi, Urusi, au hata nje ya Urusi ilibidi kufahamika na mataifa ya nje. Ama kwa kujikinga na siasa za kijamaa au kwa kujifunzia mbinu za kuukabili ubepari kwa wale waliokwishavamiwa na ubepari. Ndio lugha ya Kirusi ikajipatia umataifa wake. Ingawa umataifa wa lugha hizi za aina ya pili una namna fulani ya kulazimisha lakini ulazimishaji wake haukuwa na mabavu kama ule wa lugha za wakoloni.

Ni lugha chache sana, kama zipo, ambazo zimefanikiwa kupata hadhi ya umataifa bila ya kupitia katika mojawapo ya mikondo hiyo iliyoelezwa. Lugha ya Kiswahili nayo haikuepukana na mkumbuo huo. Lugha ya Kiswahili ilianza kujipatia hadhi ya kimataifa kwa kupewa jina lake la sasa yaani Kiswahili - jina la asili la lugha hii bado linatafutwa. Lugha hii ilipata jina hilo

kutokana na jinsi ilivyokwisha enea katika mwambao wa Afrika ya Mashariki, tangu Somalia hadi Msumbiji. Hivyo matumizi ya lugha hii yalikwishakiuka mipaka ya nchi moja na kuendelea kutumika kati ya nchi na nchi, makundi ya watu, na kadhalika.

Wananchi wa sehemu hizi za mwambao walikuwa na lugha zao zaidi ya lugha ya Kiswahili, kama wanavyoendelea kuwa nazo hivi leo. Katika hamu yao ya kutaka kushiriki katika maisha na shughuli za kibiashara za mwambao wa Afrika ya Mashariki walijikuta wanalazimika kujifunza lugha iliyofahamika ndani na nje ya mipaka ya nchi au vikundi vyao. Ndipo lugha ya KiswahiIi ikajipatia nafasi ya kujijenga kama chombo cha mataifa.

Jambo la kushangaza na la ajabu ni kwamba lugha ya Kiafrika iliachiwa iendeshe shughuli muhimu za kikabaila na za mabepari wakati ambapo lugha za makabaila na za mabepari zilikuwapo. Hali hii inajitokeza tena wakati wa biasbara ovu ya utumwa ambapo lugha iliyotumiwa kuendesha shughuli hii ilikuwa ni Kiswahili.

<u>Maswali</u>

1. a) Eleza tofauti kuu kati ya makundi mawili ya lugha za kimataifa . (alama 2)

……..….
……...…….
……...…….

b) Ni hali gani iliyosaidia kuenea kwa lugha za kundi la kwanza ? Fafanua (alama 4)

……..….
……...…….
……...…….
……..…….
……
……...…….
……
……...…….
……
……...…….
……
……...…….
……

c) Taja kwa ufupi sababu za kuenea kwa lugha za kikundi cha pili. (alama 2)

……..….

……...…….

……...…….

d) Kiswahili kilipata vipi hadhi ya kuwa lugha ya kimataifa. (alama 4)

……..….

……...…….

……...…….

……..…….

……

……...…….

……

……...…….

……

……...…….

……

……...…….

……

e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika habari (alama 3)

i) Ulikolea

……..….

ii) Majilio

……..….

iii) Mkumbo

……..….

2. **UFUPISHO**

.

Kutopanga uzazi husababisha mateso mengi na dhiki kwa mamilioni ya watu ulimwengu kote. Kwa mfano tukiangalia uchumi wa ulimwengu kwa jumla tutaona kuwa mali za kiasili kama madini, mafuta, misitu, wanyama na maji safi zinazidi kupungua. Vilevile, kiwango cha utoaji wa vyakula na mfumko wa bei ya maisha kwa jumla ni matatizo yanayoathiri sana hali zetu za maisha ya kila siku. Ni wazi kwa hivyo kuwa hapana taifa linalotaka kuona watu

wake wakifa kwa njaa, maradhi au umaskini ama wakikosa huduma muhimu kama matibabu maji safi, shule na kadhalika. Haina haja kueleza kuwa eneo la ardhi nzuri inayofaa kwa kilimo inapungua kwa kiasi watu wanavyozidi kuongezeka kwa jumla kwa hivyo tunaweza kusimamia na kutabiri kwa usahihi ongezeko hilo. Jambo hilo huwa muhali iwapo watu, hawazingatii mpango madhubuti wa kupanga uzazi.

Siyo rahisi kueleza kinagaubaga manufaa yote ambayo jamaa inaweza kupata kutokana na kutekeleza upangaji wa uzazi. Imeonyeshwa hata hivyo waziwazi kutokana na utafiti wa kisayansi kuwa mpango wa uzazi ukifuatwa kwa makini na uzingativu, huweza kusaidia kuunda jamaa yenye afya nzuri kwa upande wa mama na mtoto. Kwa mfano, mama hupata wakati wa kumnyonyesha vyema mtoto hadi umri unaofaa kumwachisha kunyonya. Pia, yeye mama hupata wasaa wa kutosha kumtunza mtoto wake na kutenda kazi zingine za nyumbani na shughuli za nje. Kufaulu kabisa kwa njia yoyote ya kupanga uzazi hutegemea mambo matatu muhimu kwa upande wa mama hasa. Mambo hayo ni afya ya mama ambayo inaweza kuathiri afya ya mtoto atakayemzaa baadaye, umri alio nao mama na idadi ya mimba alizowahi kubeba huyo mama hapo mbeleni. Kwa njia ya uchunguzi wa kisasa wa kitaalamu, matabibu wanatufahamisha kuwa kuna madhara na hasara nyingi sana ambazo humpata mama anayepata watoto wengi bila kupanga uzazi wake. Kwa mfano vifo vingi vya watoto wachanga katika mataifa machanga katika bara la Afrika, huhusishwa na kutofuata mpango wa uzazi. Wastani wa matarajio ya kipindi cha maisha katika Afrika ni miaka 49 ambacho ni cha chini sana kikilinganishwa na kile cha mataifa yaliyostawi. Isitoshe tunaelezwa kwamba watoto wachanga wapatao 149 katika kila 1000 wanaozaliwa hufa miezi michache tu baada ya kuzaliwa ambapo kati ya wanawake 110 na 647 walio katika umri wa kuzaa hufa kila mwaka katika kila idadi ya wanawake 100,000 katika bara hili.

Watoto wanaozaliwa mfululizo bila ya kipindi kirefu baina yao pia hupata madhara mengi ya kiafya. Kwa hakika wengi wa watoto kama hao hufa muda mfupi baada ya kuzaliwa. Kulingana na takwimu zilizopo sasa za kitabibu, asilimia 45 ya watoto wanaozaliwa wakiachana, kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mmoja na nusu hufa. Hali kadhalika tunafahamishwa kuwa baada ya kupata mtoto wa nne au wa tano, iwapo mama hapati muda wa kutosha wa kupumzika kabla ya kupata mimba nyingine kwa kiasi kikubwa mimba anazobeba baada ya hapo huharibika katika miezi miwili ya mwanzo na mwisho tangu kushika mamba. Vifo vingi vya kina mama kutokana na shida za uzazi hutokea miongoni mwa kina mama wenye umri mdogo wa kati ya miaka 20 na 34 na hutokea sana miongoni mwa kina mama wanaozaa mfululizo.
Maradhi mbalimbali yanayosababishwa na ukosefu wa protini kama vile kwashakoo’ maradhi ya kunyong’onyea mwili yaitwayo “Marasmus” huwashambulia sana watoto wanaozaliwa wakifuatana mfululizo. Vilevile, watoto kama wale mara nyingi hulemaa na kupoteza viungo

vyao kama mikono, miguu na hata huharibikiwa na sehemu kama vile figo na moyo kwa kukosa maziwa ya mama ambayo huachishwa kabla ya umri ufaao. Mtoto hudhoofika sana na asipopata matibabu na kinga hushikwa na maradhi kama ukambi, ndui, kupooza, kifua kikuu, pumu na mengineyo. Kwa vile mtoto kama yule huwa hana nguvu na ni myonge, yeye huweza kufa kwa ugonjwa wa kawaida kama homa.

Kwa upande wa mama, kama tulivyotangulia kueleza hapo mbeleni mama azaaye watoto wengi kwa wakati mfupi hudhoofika sana na kuwa katika hatari ya kupoteza maisha yake ama katika baa la uzazi au baadaye ama hata wakati yu mja mzito. Mama kama yule huenda asiweze kufanya kazi nyumbani ama katika shughuli za ujenzi wa taifa. Isitoshe, yeye hutatizika kuwatunza watoto wengine kwa kuzidiwa na mzigo wa kuilea mimba aliyo nayo au mtoto mchanga aliyempata. Akiwa mwenye mimba, mtoto tumboni naye hudhoofika kwa kukosa malaji bora kutoka kwa mama yake na hivyo kuhatarisha maisha yake. Mama kama huyu huwa na upungufu wa damu mwilini, haishi kuona kizunguzungu, kuumwa na kichwa na magonjwa mengine kama hayo.

a) Dondoa mambo muhimu katika aya ya kwanza. Maneno (35 – 45) (alama 5)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

b) Eleza madhara ya kuzaa watoto wengi kwa muda mfupi mfupi (maneno 60 – 70) (alama 10, 1 utiriko)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. **MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Tumia msemo ufuatao katika sentensi. (alama 1)

Fanya lele mama

……..….

b) Tunga sentensi kuonyesha tofauti ya vitate hivi. (alama 2)

i) Mjusi

……..….

ii) Mjuzi

……..….

c) Andika katika hali ya umoja . (alama 2)

i) Masaibu yaliyowapata yaliwafanya wapoteze matumaini maishani.

……..….

ii) Machaka ya waridi hayazai maua meusi.

……..….

d) Andika katika hali ya ukubwa. (alama 2)

Asiye na mwana aeleke jiwe

……..….

e) Tumia neno <u>mwitu</u> kama; (alama 3)

(i) Kivumishi

……..….

(ii) Kielezi

……..….

(iii) Nomino

……..….

f) Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali.

Wanafunzi wote wamewasili lakini wengi walichelewa sana. (alama 4)

g) Kwa kutoa mifano eleza sauti zifuatazo (alama 2)

(i) Kipasuo – kwamizo

……..….

(ii) Kitambaza

……..….

h) Eleza matumizi ya KU katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kusoma sana hakukumzuia kujiingiza kulikokuwa na wajinga.

……..….

……..….

i) Kanusha (alama 2)

Ungeipoteza kalamu yake, ungelazimishwa kuinunua nyingine.

……..….

j) Andika kwa usemi halisi . (alama 2)

Asha alimwita Halima na kumsihi waandamane kwenda kuogelea siku iliyofuata

……..….

k) Bainisha nyakati na hali zilizotumiwa katika sentensi ifuatayo. (alama 4)

"Mgeni wangu akija nitampokea kwa mikono miwili, ningekuwa na jimbi ningemchimjia" Mwanaidi alimwambia Mzee Juma.

……..….

……...…….

……...…….

……..…….

……

……...…….

……

……...…….

l) Andika sentensi hii tena bila kutumia 'amba' (alama 2)

Ng'ombe ambaye hupewa chakula kizuri ndiye ambaye hukamuliwa maziwa mengi.

……..….

……...…….

……...…….

m) Andika kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari (alama 2)

Maina <u>aliushindika</u> mlango ili <u>avue</u> sidiria.

……..….

……...…….

……...…….

n) Tambua yambwa-kitondo na yambwa-kipozi . (alama 2)

Juma aliwachemshia wageni wake chai na kisha akawapelekea mezani.

……..….

……...…….

……...…….

o) Huu ni ungonjwa gani? (alama 2)

Kifaduro;

……..….

……...…….

……...…….

p) Kwa kutoa mifano onyesha tofauti kati ya Shadda na kiimbo. (alama 2)

……..….

……...…….

……...…….

q) Eleza matumizi mawili ya:

Ritifaa (alama 2)

……..….

……...…….

……...…….

r) Eleza maana mbili za sentensi hii:

Mzee huyu anaogopa magonjwa zaidi ya vijana. (alama 2)

……..….

……...…….

……...…….

4. ISIMU JAMII

Chenga moja, chenga mbili, Kombora-

……goooo ! Fantastic ! Ajabu !

Msilikilizaji, Uwanja wote umesimama; Shangwe, vigelegele, hoihoi; Sijui nisemaje. Mnamo dakika ya tisini vijana wa nyumbani …. Na refa amepuliza kipenga na mpira umekwisha !

a) Taja rejesta ya dondoo hii. (alama 1)

……..….

……...…….

……...…….

b) Taja sifa nne za lugha ya rejesta hii ambazo zimejidhihirisha katika dondoo (alama 4)

……..….

……...…….

……...…….

c) Taja sifa zingine mbili za lugha ya rejesta hii zilizo katika dondoo hii. (alama 2)

……..….

……...…….

……...…….

d) Eleza maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumiwa katika isimujamii. (alama 3)

i) Misimu

……..….

ii) Lakabu

……..….

iii) Pijini

……..….